KCSE ACHIEVERS PREDICTION

Kenya Certificate of Secondary Education

102/2
Karatasi ya 2
KISWAHILI
LUGHA
Muda: Saa 2 ½

Jina: ..... Nambari ya Mtahiniwa .....

Sahihi ya Mtahiniwa ..... Darasa .....

Maagizo

(a) Andika jina lako na namba yako ya usajili katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(b) Tia sahihi yako kisha uandike darasa lako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
(c) Jibu maswali **yote.**
(d) Majibu yote yaandikwe kwenye nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
(e) Majibu yote ni **lazima** yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.
(f) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.

KWA MATUMIZI YA MTAHINI PEKEE: -

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

1. **UFAHAMU**

Ratiba ya siku hiyo ilipokuwa ikiendelea,machozi yalimlengalenga Ghamu hata akawa na ukungu mbeleni mwake asiweze kuona mbele. Kilichomtia huzuni zaidi ni usuhuba wake wa karibu na Zawadi. Alianza kukumbuka maisha yao ya awali na Zawadi. Alikumbuka walipoanza pamoja masomo katika shule ya chekechea. Walitembea hatua kwa hatua masomoni. Walikwea vidato vya masomo pamoja. Walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Urafiki wao ulikuwa ule ambao mmoja akijikwaa mwingine anahisi uchungu. Zawadi na Ghamu walipendana kwa kweli.

Ghamu alikumbuka walipofanya mtihani wao wa kuhitimu katika shule ya msingi. Ilikuwa sadfa kwao kwani matokeo yalipotangazwa walijipata katika shule moja ya upili. Fauka ya hayo, hatimaye, walijiunga katika chuo kikuu kimoja na kuishia kufanya kozi moja. Sasa Ghamu anaghubikwa na huzuni zaidi anapokumbuka hayo yote.

" Pandeni gari hili la kifahari twende zetu. Hii ni bahati yenu. Bahati huja tu mara moja. Pandeni gari warembo. Kwa nini wasichana warembo kama nyinyi wapigwe na jua. " Ghamu alikumbuka maneno ya mzee yule aliyejitambulisha kama Mzito. Zawadi alikuwa ameketi na rafikiye, Ghamu, kwenye bustani ya Hewa. Ilikuwa mazoea yao kuenda kupunga hewa katika mazingira hayo wikendi. Mzee mmoja alishusha kioo cha gari lake aina ya Mercedes Benz. Gari hilo lilikuwa jipya kabisa. Zawadi na Ghamu walidinda kuingia ila mzee yule wa umri wa miaka kama sabini hivi alisema. Alikuwa na upara na mvi kwenye sehemu ndogo ya kichwa kilichokuwa na nywele.

Mzee yule alizidi kujaribu kuwashawishi mabinti hawa. Ushawishi wa Mzito ulifua dafu Zawadi alipomwashiria Ghamu waingie garini. Hii ni baada ya mzee kuwaahidi kuwapeleka hoteli ya kifahari wale na kunywa. Ghamu alishangazwa na uamuzi wa Zawadi. Alijaribu kumshauri asiingie kwenye gari hilo lakini Zawadi alitia sikio nta. Hatimaye, Ghamu alikataa katakata na Zawadi akaingia kwenye gari lile. Zawadi alipungia mkono na kumwambia, " ishi kwa ufukara wako, mimi sasa ninauaga.

Tangu siku hiyo, maisha ya Zawadi ilibadilika. Alipangiwa jumba la kifahari jijini. Akanunuliwa nguo mpya za kifahari. Kila siku alivalia nguo mpya alipoingia darasani. Si sketi, si suruali

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

ndefu, si viatu. Alijitia vipodozi ainati. Alisuka mitindo mbalimbali ya nywele. Alikula katika hoteli za kifahari. Kila wikendi,hawakwenda tena bustani ya Hewa kama ilivyokuwa ada yao. Alienda visiwa vya Lamu, Kwale, Mombasa na maeneo mengine ya kifahari. Maisha haya yalimtenga na Ghamu kama mbingu na ardhi. Kila alipomwona Ghamu, Zawadi alimtazama kwa bezo.

" Unamjua msichana anayeitwa Zawadi? " Ghamu aliambiwa kwa simu. Awali hili lilimtia kiwewe. Alipojibu kuwa anamjua, alifahamishwa kuwa mwili wake umepatikana kule Mto Yala. Habari hizo zilisambaa sana katika mitandao ya kijamii hata zikawafikia wazaziwe Zawadi bila hodi. Huzuni ilitanda. Zawadi alikuwa mtoto wa pekee kwa wazazi wao. Alikuwa nyota yao.

Uchunguzi ulifanywa na kubaini kuwa Zawadi alikuwa ameuawa, viungo vyake vya mwili kutolea na kupelekwa kusikojulikana. Mzito alidaiwa kuwa alikuwa raia wa nchi nyingine aliyekuwa Kenya kwa njia isiyokuwa halali. Alikuwa keshatoroka baada ya kutenda unyama ule.

MASWALI

a) Yape masimulizi haya anwani mwafaka. (alama 1)

……

b) Zawadi na Ghamu walikuwa marafiki wa dhati. Thibitisha. (alama 2)

……
……

c) Tamaa mbele mauti nyuma. Tetea ukweli wa kauli hii kwa kurejelea kifungu hiki. (alama 4)
……
……
……
……
.

d) Eleza kwa hoja **tatu** kinaya kinachojitokeza katika kifungu hiki. (alama 3)

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

……
……
……
……..

e) Eleza jinsi mabadiliko yanavyojitokeza katika masimulizi haya. (alama 2)

……
……
……
……

f) Fafanua matumizi ya taswira onevu katika kifungu hiki. (alama 1)

……
……

g) Eleza maana ya kauli zifuatazo kama zilivyotumiwa na mwandishi : (alama 2)

i) anapoenda mbele ya haki

……

ii) aligubikwa

……

2. UFUPISHO

Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.

Kila msanii anacho kifaa chake ambacho anakitumia, ambacho kinakuwa alama ya usanii wake. Mchoraji anategemea sana kalamu au rangi zake na mchongaji anao ubao au mti wake. Vivyo hivyo mwanafasihi naye anategemea lugha katika usanii wake. Matumizi ya lugha ni miongoni mwa mambo muhimu yanayotofautisha kazi ya fasihi na kazi isiyo ya fasihi. Jinsi ambavyo mwandishi anavyoitumia lugha yake na kiwango cha usanii anachofurahia ndivyo alama muhimu inayomtofautisha na mwandishi mwingine wa fasihi.

Katika uhakiki wa kazi za fasihi za hivi karibuni, hasa katika Kiswahili, kumekuwa na msisitizo mkubwa katika maudhui ya kazi hizo au kwa lugha rahisi, ujumbe unaotolewa na mwandishi. Hivyo maswali yanayoulizwa ni kama: Kazi hii ina umuhimu gani katika jamii ya leo? Inajengaje tabia, mwenendo na mwelekeo wa jamii? Ina maadili gani?

Mara nyingi, wahakiki hawaulizi mwandishi alivyofaulu kisanaa isipokuwa kama jambo la ziada tu mwishoni. Uhakiki wa namna hii hasa umehusu kazi za fasihi zisizo za ushauri, kwa sababu imekubalika kwa muda mrefu kuwa mshauri ni lazima aitawale lugha yake vizuri ndipo aweze kuleta ule mvuto maalum unaotakiwa na kufikia viwango vinavyokubalika katika fani hii.

Haiwezekani kutenganisha maudhui na usanii katika kazi yoyote ile ya fasihi. Ujumbe unaoletwa katika kazi ya fasihi unaweza kutolewa na mtu mwingine yeyote kwa njia nyingine. Ujumbe huo unaweza kutolewa kwa njia ya hotuba, vitabu au maongezi ya kawaida.

Katika isimu ya lugha, tunaposema ya kwamba mwanadamu anajua lugha yake, tuna maana kuwa "amemeza" mfumo wa lugha yake wa matamshi, muundo wa maneno, muundo wa sentensi na maana zinazokusudiwa. Ujuzi alio nao mwanadamu huyu ni sawa, na ujuzi walionao wanadamu wengine wa jamii yake wanaozungumza lugha moja. Hivyo tukisema kuwa mwanadamu aongee lugha. hatuna maana tu ya kule kumeza mfumo wake wa lugha bali ni uwezo wake wa kuitumia katika mahusiano yake na wanajamii wengine. Katika lugha yoyote ile kuna mitindo mingi inayotumika kutegemea kile kinachozungumziwa.Hivyo, tunaweza kuwa na mtindo wa siasa, sheria dini na kadhalika. Pia upo mtindo wa kawaida unaotumika.

Katika mawasiliano ya kila siku ya wanajamii moja, katika mtindo huu, kuna matumizi ya aina mbalimbali yakihusiana na nyanja tofauti za maisha. Matumizi haya yanaitwa rejesta kwa lugha ya kitaalam. Rejesta yoyote ile inategemea nani anazungumza nini na nani, wapi kuhusu nini na kwa sababu gani.

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

Mtu anayejua lugha yake vizuri, tunategemea aweze kuitumia katika mitindo iliyobadilika na aweze kujua mazingira anayopaswa kutumia mtindo mmoja badala ya mwingine. Katika mahusiano ya kawaida, mtumiaji wa lugha anapaswa kujua ni rejesta gani anapaswa kutumia kila wakati. Mwandishi wa habari lazima awe "amefuzu" katika kuweka haya matumizi tofauti ya lugha.

Mwandishi huyu anatakiwa kuwa mtafiti ili ajue yale matumizi ambayo yeye hana haja nayo katika mahusiano yake ya kawaida na huyo aweze kuchora jamii yake inayostahili katika kazi yake. Sababu kubwa ya kumtaka mwanafasihi kuyajua kinaganaga matumizi tofauti ni ule ukweli kuwa kazi ya fasihi haina mpaka na utumizi wa lugha.

Maswali.

(a) Eleza kwa nini lugha ni kipengele muhimu katika uwasilishaji wa fasihi(maneno 70-80) (alama 8)

Nakala ya matayarisho

……

……

……

……

……

……

……

……

……

Nakala safi

……

……

……

……

……

……
……
……
……

(b) Fupisha aya tatu za mwisho(maneno 75-85) (alama 7)

Nakala ya matayarisho

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

Nakala safi

……
……
……
……
……
……
……
……
……
……

3. **MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Linganua sifa za konsonanti katika neno: ng'ofoa. (alama 3)

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

……

……

(b) Bainisha silabi katika neno lifuatalo: nge (alama 1)

……

(c)Bainisha silabi inayowekwa shadda katika maneno yaliyokolezwa wino. (alama 2)

Ala! **Barabara** iliyokarabatiwa kwa **ala** za kisasa ina **walakini**.

……

……

(d) Ainisha sentensi ifuatayo kwa kuzingatia dhima yake. (alama 1)

Meno yote yameng'oka.

……

(e) Andika neno lenye muundo ufuatao.

(i) kiambishi kikanushi cha nafsi ya tatu umoja, kikanushi cha wakati uliopita, yambwa, mzizi, kauli tendea, kauli tenda (alama 1)

……

(ii) wingi (ngeli ya U – ZI), mzizi, kiishio (alama 1)

……

(f) Tunga sentensi ukitumia kitenzi –cha- katika wakati ujao hali timilifu.(kauli tendewa) (alama 2)

……

(g) Andika upya sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendesha kwa kuzingatia maneno yaliyopigwa mstari. (alama 2)

Mama alimfanya <u>anawe</u> mikono kwa maji baridi yaliyomfanya <u>aogope.</u>

……

……

(h)Tunga sentensi ukitumia nomino kutokana na kitenzi: tafakari. (alama 2)

……

(i) Eleza jinsi viambishi vilivyopigiwa mstari vilivyotumiwa katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

"Simame<u>ni</u>!" mwalimu a<u>ka</u>amuru, "ninyi <u>ndi</u>nyi wanafunzi walio<u>ji</u>kimbiza uwanjani?" akawauliza.

……
……
……
……

(j) Kando na herufi ndogo, eleza matumizi mawili ya kiakifishi kilichotumika katika kirai nomino kifuatacho. (alama 2)

ng'ombe wawili

……
……

(k) Andika upya sentensi zifuatazo kulingana na maagizo yaliyo mabanoni.

(i) Mwanafunzi aliyeadhibiwa jana aliiba vitabu vya wenzake. (andika sentensi mbili sahili kutokana na sentensi hii) (alama 2)

……
……

(ii) **Ukiadilika** utajiepusha na **kuwadhulumu** wengine. (Iandike sentensi upya ukitumia vivumishi vya sifa vilivyotokana na vitenzi vilivyokolezwa wino.) (alama 2)

……
……

(iii) Vile vyenye alisema sikuelewa juu hadi sikusikia. (sahihisha) (alama 1)

……
……

(l) Bainisha yambwa, kiarifu na chagizo katika sentensi ifuatayo. (alama 4)

Cheworei alibebewa mizigo kwa punda.

……
……
……

(m)Changanua kwa njia ya mistari. (alama 3)

Yule mwanariadha aliyepata ajali alipendwa na wengi.

……
……

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

……

……

……

(n) Ainisha virai katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Vile viwili vililetwa na mwalimu wa Kiswahili.

……

……

(o) Tumia kihusishi cha mtenda katika sentensi. (alama 1)

……

(p) Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo. (alama 2)

Mlango unafungika.

……

……

……

(q) Chakaa ni kwa zeeka. _____ ni kwa bahati, _____ni kwa linda. (alama 1)

(r) Andika uyakinisho wa sentensi ifuatayo. (alama 1)

Usiponieleza sitakupa.

……

(s) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya: **fuja** na **vuja**. (alama 2)

……

……

4. ISIMUJAMII

(a) Eleza namna kaida zifuatazo zinaathiri matumizi ya lugha katika jamii.

(alama 4)

(i) tabaka

……

……

(ii) uana

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme

……

……

(b) Ningependa kutoa maoni yangu ya kuunga mkono mswada uliowasilishwa katika kikao hiki na Mheshimiwa Obongita. Mswada huu, ikiwa utaidhinishwa, utachangia kupunguza uharibifu wa Ozone Layer, ambao huchangia madhara mengi kwa mwili wa binadamu. Kumbuka, mheshimiwa spika, katiba yetu, katika kifungu cha 140 ibara ya 5 (a), inamhakikishia kila raia haki ya kuishi katika mazingira safi. This is a right for every citizen. Sadakta.

(i) Tambua sajili hii. (alama 1)

……

……

(ii) Eleza sifa za sajili hii kama zinavyojitokeza katika kifungu hiki. (alama 5)

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

©The Kenya National Examinations Council
Contact 0724333200/ 0795491185/ 0768321553 Marking Scheme